WIZARA YA NISHATI

# NewsBulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 59 | Oct 1 - 30 2024



# DKT.MPANGO ATAKA AFRIKA KUUNGANISHA NGUVU UENDELEZAJI WA JOTOARDHI

WIZARA YA NISHATI +255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**
Dkt. James Mataragio
Dkt. Khatibu Kazungu

**MHARIRI**
Neema Chalila Mbuja
Prudence Constantine

**WAANDISHI**
Theresa Mhagama
Hafsa Omary
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Immaculate Makilika
Amanzi Kimonjo

**WAPIGA PICHA**
Steven Nyamiti
Henry Kilasila
Mustafa Shahame
Isaya Mwakajana

**MSANIFU KURASA**
Brian Mbaga

© NISHATI 2024

# DKT.MPANGO ATAKA AFRIKA KUUNGANISHA NGUVU UENDELEZAJI WA JOTOARDHI

- Aeleza umuhimu wa Sekta Binafsi kuhusishwa uendelezaji Jotoardhi
- Akaribisha uwekezaji katika vyanzo vya Jotoardhi Tanzania
- Kapinga amshukuru Dkt.Samia kwa Dira inayoiimarisha Sekta ya Nishati



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Isdor Mpango akifungua Kongamano la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) jijini Dar es Salaam tarehe 23 Oktoba, 2024.



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga akizungumza wakati wa hafla ya ufunguzi Kongamano la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) jijini Dar es Salaam tarehe 23 Oktoba, 2024.

Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango amesema Bara la Afrika linapaswa kuunganisha nguvu na kushirikiana ili kuweza kuendeleza ipasavyo nishati ya Jotoardhi ambayo ni safi na endelevu na kuondokana na nishati zisizo safi katika kuzalisha umeme ikiwemo mafuta mazito.

Dkt.Mpango amesema hayo jijini Dar es Salaam tarehe 23 Oktoba, 2024wakati akifungua Kongamano la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) ambalo limehudhuriwa na washiriki 800 kutoka nchi 21 duniani.

Aidha, amesema kila nchi inapaswa kuwa na Taasisi maalum kwa ajili ya kusimamia uendelezaji wa Nishati ya Jotoardhi na kuwa na kanuni nasheria madhubuti zitakazowezesha sekta binafsi kushiriki katika uendelezaji wa nishati hiyo.

Vilevile ameziasa nchi zenye Nishati ya Jotoardhi kufanya mazungumzo ya kimkakati na Taasisi za kifedha ikiwemo Mabenki ili kupata fedha za kuendeleza nishati hiyo kutokana kuhitaji fedha nyingi katika uendelezaji wake badala ya kutegemea bajeti za Serikali pekee.

Amesema mipango ya Tanzania ni kuwa na umeme wa kiasi cha zaidi ya megawati 5000 ifikapo mwaka 2030 kutoka vyanzo mchanganyiko huku nishati jadidifu ikipewa kipaumbele ikiwemo Jotoardhi, upepo na Jua.

Ameeleza kuwa, Tanzania iliamua kwa vitendo kuendeleza nishati ya Jotoardhi kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuanzisha Taasisi inayosimamia sekta husika mwaka 2014 ambayo moja ya kazi zake ni kusimamia uendelezaji wa nishati hiyo.

Amesema tayari Tanzania imekamilisha utafiti wa awali kwenye baadhi ya maeneo matano yenye viashiria vya Jotoardhi kwenye Bonde la Ufa na sasa kuna uchorongaji unaoendelea katika eneo la Ngozi ili kuhakiki uwepo wa nishati hiyo.

Ameongeza kuwa, hatua nyingine iliyopigwa kwenye Jotoardhi nchini ni kuongezeka kwa idadi ya wataalam waliobobea katika masuala ya nishati hiyo na ununuzi wa rig itakayotumika kwa ajili ya shughuli za uchorongaji kwenye maeneo yenye mashapo ya Jotoardhi.

Amewashukuru Wadau mbalimbali wa maendeleo wa wanaoiunga mkono Tanzania kifedha na kiufundi ili kuendeleza nishati ya Jotoardhi ikiwemo Japan, Iceland na Ireland.

Katika kongamano hilo, Dkt. Mpango amewakaribisha Wawekezaji ili kuendeleza nishati ya Jotoardhi katika vyanzo mbalimbali ikiwemo Ngozi (70MW), Kiejo-Mbaka (60MW), Songwe (kati ya 5 na 35MW), Natron (60MW) na Ruhoi (5MW).

Pia amekaribisha washiriki wa ARGeo-C10 kufanya uwekezaji kwenye sekta mbalimbali ikiwemo ya madini na kufanya utalii katika vivutio mbalimbali ikiwemo Mlima Kilimanjaro, Serengeti, Ngorongoro n.k

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais, Capt. George Mkuchika amesema chini ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan sekta ya nishati imezidi kupiga hatua ambapo umeme vijijini umefika kwa takriban asilimia 98 na ifikapo Desemba mwishoni vijiji vyote vitakuwa vimesambaziwa.

Ameeleza kuwa hali hiyo ni kielelezo cha mahitaji ya umeme kuongezeka hivyo lazima uendelezaji wa vyanzo mchanganyiko vya nishati uongezeke ikiwemo Jotoardhi ambayo ikiendelezwa itaweza kuzalisha umeme wa megawati 5000.

Kwa upande wake, Waziri wa Nishati na Mafuta kutoka Kenya, James Wandayi amesema kuwa nchi hiyo tayari imepata mafanikio katika nishati ya Jotoardhi kwani kwa sasa zaidi ya asilimia 45 ya umeme nchini humo unazalishwa na Jotoardhi.

Amesema Nishati ya Jotoardhi inapaswa izidi kupigiwa chapuo barani Afrika kutokana na kuwa ni endelevu ambapo licha ya kutumika kuzalisha umeme inatumika pia kwenye sekta nyingine ikiwemo kilimo na ufugaji.

Awali, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga alimshukuru Rais, Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kujitoa kwake katika kuendeleza Sekta ya Nishati na uongozi wake unaotoa Dira katika kushughulikia masuala mbalimbali yanayohusu Sekta.

Amesema Jotoardhi itawezesha azma ya Tanzania kuwa na umeme unaotokana na vyanzo mchanganyiko huku lengo likiwa ni kuzalisha kiasi cha megawati 995 kutokana na nishati hiyo ifikapo mwaka 2024 hali itakayoongeza pia usalama wa gridi ya umeme.

Amesema nishati ya Jotoardhi ni suluhisho muhimu katika utatuaji wa changamoto za upatikanaji wa nishati ya kutosha barani Afrika ambayo inaenda sambamba na mipango ya dunia katika kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa.

Hafla ya ufunguzi wa Kongamano la ARGeo-C10 imehudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwemo Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wabunge, Mabalozi wa nchi mbalimbali, Madiwani, Wadau wa Maendeleo na Watendaji kutoka Taasisi za Serikali na Binafsi



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Isdor Mpango (kushoto) akipokea ramani inayoonesha viashiria vya jotoardhi nchini baada ya kufungua Kongamano la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) jijini Dar es Salaam tarehe 23 Oktoba, 2024. Anayemkabidhi ni Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Isdor Mpango (katikati) akiingia katika ukumbi wa mikutano katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) kabla ya kufungua Kongamano la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) tarehe 23 Oktoba, 2024.

# DKT. BITEKO AKARIBISHA WAWEKEZAJI SEKTA YA NISHATI

- Ataja Mikakati ya Serikali Kuimarisha Sekta ya Nishati
- Aeleza Namna Tanzania Inavyojiandaa Kuuza Umeme nchi Jirani na Uwepo wa Soko la Uhakika
- Asema Ushiriki wa Sekta Binafsi ni Muhimu kwa Maendeleo ya Nchi
- Ashiriki Wiki ya Kimataifa ya Nishati Singapore, Ashukuru kwa Mwaliko na Kuelezea Mafanikio ya Sekta ya Nishati Tanzania



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk Doto Biteko akizungumza wakati akishiriki mjadala kuhusu nishati, wakati wa ufunguzi wa Wiki ya Kimataifa ya Nishati nchini Singapore tarehe Oktoba 21, 2023.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa Serikali inawakaribisha wawekezaji katika sekta ya nishati ili kuongeza kasi ya usambazaji, uzalishaji na unganishwaji wa nishati nchini Tanzania.

Dkt. Biteko amesema hayo leo Oktoba 21, 2023 nchini Singapore wakati akishiriki mjadala kuhusu nishati akiwa pamoja na Waziri wa Madini na Nishati kutoka nchini Cambodia, Mhe. Keo Rottanak na Waziri wa Maliasili kutoka nchini New Zeland Mhe. Shane Jones wakati wa ufunguzi wa Wiki ya Kimataifa ya Nishati ya nchini Singapore.

" Serikali haziwezi kufanya kila kitu zenyewe hivyo ni muhimu kushirikiana na sekta binafsi. Sisi Tanzania tunawaalika sekta binafsi ije kuwekeza katika sekta ya nishati kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji, upatikanaji na usambazaji nishati na kuboresha maisha ya watu kwa ujumla," amesema Dkt. Biteko.

Akizungunzia, ajenda ya nishati safi ya kupikia nchini amesema kuwa ni matokeo ya utafiti uliofanywa na kubaini kuwa idadi kubwa ya Watanzania wanatumia kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia hali inayosababisha magonjwa ya mfumo wa upumuaji na uharibifu wa mazingira.

Ili kupunguza athari hizo, Dkt. Biteko amesema kuwa Serikali imeandaa mkakati unaolenga kuhakikisha Watanzania asilimia 80 wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

" Serikali imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na kuhakikisha nishati safi inapatikana kwa urahisi na bei nafuu na hivyo tunawakaribisha wawekezaji kuja kuwekeza katika hili kwa sababu soko lipo," amesema Dkt. Biteko.

Kuhusu jitihada za Serikali za kuimarisha sekta ya nishati nchini, Dkt. Biteko ametaja miradi mbalimbali inayofanywa na Serikali ikiwemo mradi wa kufua umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2115.

" Serikali inaendeleza vyanzo vipya vya nishati mfano umeme wa jua, upepo na gesi, aidha kwa sasa asilimia 51 ya umeme unazalishwa kwa maji. Tanzania tumeendelea na maandalizi ya kuziuzia umeme nchi za Kenya, Rwanda, Burundi na sasa tunaendelea na mradi kwa

ajili ya kuunganisha na nchi ya Zambia, kupitia Umoja wa Mauzio ya Umeme wa pamoja katika nchi za Afrika Mashiriki na Jumuiya za Kusini mwa Afrika (SADC) tuna soko la uhakika na hivyo tunawakaribisha wawekezaji kuja kushirikiana nasi," amesisitiza Dkt. Biteko.

Naye, Waziri wa Madini na Nishati kutoka nchini Cambodia, Mhe. Keo Rottanak amesema kuwa mwaka 1998 nchi yake ilifanya mageuzi makubwa katika sekta ya nishati na kuwa sasa asilimia 99 ya vijiji ina umeme.

" Tutahakikisha tunafikisha umeme katika nyumba za watu na malengo yetu ni ifikapo mwaka 2030 umeme unaozalishwa kwa jua kuwa mbadala wa umeme unaozalishwa na maji, amesema Mhe. Rottanak.

Kwa upande wake, Waziri wa Maliasili na kutoka nchini New Zeland, Mhe. Shane Jones amesema kuwa nchi yake imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya kusambaza umeme na kuwa inajikita katika kuwekeza katika vyanzo mbadala vya kuzalisha nishati.

Awali akifungua mkutano huo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Viwanda na Biashara wa Singapore Mhe. Gan Kim Yong amesema kuwa mahitaji ya nishati duniani yanazidi kuongezeka siku hadi siku hivyo nchi zinapaswa kubuni vyanzo mbadala na kupunguza madhara yatokanayo na gesi ya ukaa ifikapo mwaka 2050.

Akitoa uzoefu wa nchi yake kwenye kuongeza vyanzo mbadala vya nishati amesema " Kwa sasa tuko kwenye mkakati wa kuzalisha umeme kwa kutumia haidrojeni na nyuklia ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na kuongezeka kwa ushiriki wa Kampuni za Google na Amazon ambazo zimeonesha nia ya kuwekeza kwenye miradi ya nishati jadidifu." Amesema Mhe. Kim Yong.

Aidha,katika mkutano huo pia umefanyika uzinduzi wa tawi la ofisi ya kanda ya Shirika la Kimataifa la Nishati (IEA) nchini Singapore.






# KAPINGA AIHAMASISHA DUNIA KUSHIRIKI DURU YA TANO YA VITALU VYA GESI ASILIA TANZANIA

- Ni kupitia Mkutano wa Wiki ya Mafuta Afrika
- Aeleza jinsi Sheria za Tanzania zinavyowiana na mazingira ya uwekezaji
- Asema Tanzania ina miundombinu wezeshi ya usafirishaji bidhaa za mafuta na Gesi Asilia
- Aeleza miradi inayotoa hakikisho la uwepo wa umeme wa kutosha
- Asisitiza Nishati Safi ya Kupikia ni ajenda ya nchi

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe.Judith Kapinga amesema Serikali kupitia Wizara ya Nishati itaanza zoezi la kunadi vitalu 24 vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia mwezi Machi 2025 katika kipindi cha Kongamano na Maonesho ya Mafuta na Gesi Asilia Afrika Mashariki yatakayofanyika nchini.




Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga akiuhutubia washiriki wa Kongamano la Wiki ya Mafuta Afrika (Afrika Oil Week 2024) lilifanyika nchini Afrika Kusini, Tarehe 10 Oktoba 2024, ambalo lilihudhuriwa na washiriki kutoka nchi 70 duniani kwa lengo la kujadili masuala yanayohusu mafuta na gesi asilia.

Mhe. Judith Kapinga amesema hayo wakati akihutubia Kongamano la Wiki ya Mafuta Afrika linalofanyika nchini Afrika Kusini ambalo limehudhuriwa na washiriki kutoka nchi 70 duniani kwa lengo la kujadili masuala yanayohusu mafuta na gesi asilia.

Kapinga amesema katika duru la tano la kunadi vitalu vya gesi asilia, Wizara ya Nishati imejipanga kuvitangaza vitalu vyote 24 ambapo visima 21 vipo Bahari ya Hindi na vingine vipo ziwa Tanganyika.

Ameeleza kuwa, shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini zilianza miaka ya 1950 ambapo hadi sasa kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa ni takriban futi za ujazo Trilioni 57.

Amesema gesi asilia inatumika kwa ajili ya uzalishaji wa umeme, nishati katika magari, viwandani na majumbani huku lengo likiwa ni kuendana na ajenda ya kimataifa ya mabadiliko ya nishati pamoja na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia.

Kuhusu Nishati Safi ya Kupikia, amesema hiyo ni ajenda ya nchi na kinara wake ni Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye anashirikiana na wadau wengine kuhakikisha lengo lililokusudiwa linafikiwa.

Kupitia mkutano huo, Mhe. Kapinga ameeleza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo nchini kupitia Wizara ya Nishati pamoja na kuwaalika wawekezaji kuwekeza nchini.

Amesema Serikali ya Tanzania itaendelea kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali ikiwemo utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

Kuhusu sekta ya umeme, Kapinga amebainisha miradi inayofanyika nchini kwa ajili ya kuimarisha gridi ya Taifa, ikiwemo mradi wa umeme Jua Kishapu, mradi wa Julius Nyerere utakaozalisha megawati 2,115 pamoja na miradi mingine ikiwemo ya upepo ili kuhakikisha gridi inaimarika.

Akizungumzia uwepo wa mazingira bora ya uwekezaji nchini, Kapinga amesema Serikali imeshapitia Sheria ya Petroli na mkataba kifani wa uzalishaji na ugawanaji mapato kwa lengo la kuhakikisha masharti ya kiuchumi na kisheria yanakuwa na usawa kiushindani katika sekta ya mafuta kwenye ngazi ya kikanda na kimataifa.




Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi na wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na taasisi zake wakati wa Kongamano la Wiki ya Mafuta (Afrika Oil Week 2024) lililofanyika Nchini Afrika Kusini, Tarehe 10 Oktoba 2024.

Aidha, amewaeleza washiriki wa kongamano kuhusu mifumo ya kisheria yenye uwiano kwa kuzingatia mazingira ya uwekezaji.

Vilevile, Kapinga amewahamasisha wawekezaji kuja kuwekeza Tanzania kutokana na uwepo wa miundombinu wezeshi ambayo inarahisisha usafirishaji wa bidhaa za mafuta na gesi asilia ikiwemo bomba la gesi asilia kutokea Mtwara hadi Dar es Salaam, mitambo mitatu ya kuchakata gesi asilia, bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki na bomba la mafuta kutoka Tanzania hadi Zambia.

Viongozi wengine waliohudhuria Kongamano hilo ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio, Kamishina wa Petroli na Gesi, Godluck Shirima; Mwenyekiti wa Bodi ya TPDC, Balozi Ombeni Y. Sefue Mwenyekiti wa Bodi ya PURA, Halfani Halfani, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Mha. Charles Sangweni pamoja na viongozi na wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na taasisi zake.

Kapinga amesema katika duru la tano la kunadi vitalu vya gesi asilia, Wizara ya Nishati imejipanga kuvitangaza vitalu vyote 24 ambapo visima 21 vipo Bahari ya Hindi na vingine vipo ziwa Tanganyika.

Ameeleza kuwa, shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini zilianza miaka ya 1950 ambapo hadi sasa kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa ni takriban futi za ujazo Trilioni 57.

Amesema gesi asilia inatumika kwa ajili ya uzalishaji wa umeme, nishati katika magari, viwandani na majumbani huku lengo likiwa ni kuendana na ajenda ya kimataifa ya mabadiliko ya nishati pamoja na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia.

Kuhusu Nishati Safi ya Kupikia, amesema hiyo ni ajenda ya nchi na kinara wake ni Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye anashirikiana na wadau wengine kuhakikisha lengo lililokusudiwa linafikiwa.

Kupitia mkutano huo, Mhe. Kapinga ameeleza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo nchini kupitia Wizara ya Nishati pamoja na kuwaalika wawekezaji kuwekeza nchini.

Amesema Serikali ya Tanzania itaendelea kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali ikiwemo utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

Kuhusu sekta ya umeme, Kapinga amebainisha miradi inayofanyika nchini kwa ajili ya kuimarisha gridi ya Taifa, ikiwemo mradi wa umeme Jua Kishapu, mradi wa Julius Nyerere utakaozalisha megawati 2,115 pamoja na miradi mingine ikiwemo ya upepo ili kuhakikisha gridi inaimarika.

Akizungumzia uwepo wa mazingira bora ya uwekezaji nchini, Kapinga amesema Serikali imeshapitia Sheria ya Petroli na mkataba kifani wa uzalishaji na ugawanaji mapato kwa lengo la kuhakikisha masharti ya kiuchumi na kisheria yanakuwa na usawa kiushindani katika sekta ya mafuta kwenye ngazi ya kikanda na kimataifa.

Aidha, amewaeleza washiriki wa kongamano kuhusu mifumo ya kisheria yenye uwiano kwa kuzingatia mazingira ya uwekezaji.

Vilevile, Kapinga amewahamasisha wawekezaji kuja kuwekeza Tanzania kutokana na uwepo wa miundombinu wezeshi ambayo inarahisisha usafirishaji wa bidhaa za mafuta na gesi asilia ikiwemo bomba la gesi asilia kutokea Mtwara hadi Dar es Salaam, mitambo mitatu ya kuchakata gesi asilia, bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki na bomba la mafuta kutoka Tanzania hadi Zambia.

Viongozi wengine waliohudhuria Kongamano hilo ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio, Kamishina wa Petroli na Gesi, Godluck Shirima; Mwenyekiti wa Bodi ya TPDC, Balozi Ombeni Y. Sefue Mwenyekiti wa Bodi ya PURA, Halfani Halfani, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Mha. Charles Sangweni pamoja na viongozi na wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na taasisi zake.

# DKT.BITEKO ATAKA UMOJA, USHIRIKIANO NA UBUNIFU TAASISI ZA NISHATI

- Asema Rais Samia anataka Ubunifu ili kusogeza huduma bora kwa wananchi
- Asisitiza utendaji kazi umuangalie Mtanzania wa kawaida anayeitegemea Serikali kubadili maisha
- Aagiza kila Taasisi kuwa na Vigezo vya Upimaji Utendaji Kazi
- Ataka Watendaji waache alama ya kazi, si kulinda vyeo



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt.Doto Biteko jijini Dodoma akizungumza wakati wa kikao chake na Menejimenti ya Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini yake ambacho ni cha pili kutoka uanzishwe mfumo mpya ndani ya Wizara na Taasisi zake wa kujifanyia tathmini ili kuona namna inavyofanya kazi ya kuhudumia wananchi.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewataka Watendaji na Watumishi katika Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati kuwa na umoja, ushirikiano na ubunifu ili kusogeza huduma bora kwa wananchi ikiwemo za umeme, mafuta, na Nishati Safi ya Kupikia.

Amesema hayo tarehe 28 Oktoba, 2024 jijini Dodoma wakati wa Kikao chake na Menejimenti ya Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini yake ambacho ni cha pili kutoka uanzishwe mfumo mpya ndani ya Wizara na Taasisi zake wa kujifanyia tathmini ili kuona namna inavyofanya kazi ya kuhudumia wananchi.

"Ikumbukwe kuwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wote amekuwa akisisitiza kuwepo na ubunifu kwenye Wizara na Taasisi ili kusogeza huduma za uhakika kwa wananchi na huduma hizo bora haziwezi kutokea kama hakuna umoja na ushirikiano ndani ya Taasisi za Serikali." Amesema Dkt. Biteko

Katika Kikao hicho, Dkt. Biteko amewataka watendaji wa Wizara na Taasisi kufanya kazi kwa bidii na weledi huku wakimuangalia mtanzania wa kawaida anayetegemea mipango ya Serikali ili kuweza kubadili maisha yake na kukumbuka kuwa Sekta ya Nishati ni injini ya uchumi wa nchi hivyo inapotetereka yanatokea matatizo kwenye nyanja zote za kiuchumi na hali ya maisha ya watu.

Vilevile amewakumbusha watendaji wa Wizara na Taasisi kutochukua muda mwingi kulinda vyeo bali kinachotakiwa ni matokeo ya kazi zitakazoacha alama kwenye Taasisi kwani vyeo huwa havidumu.

Pamoja na kupongeza Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa kuwa na mchango katika ukuaji wa uchumi wa nchi, ametaka kila Taasisi kuwa na Vigezo vya Upimaji wa Utendaji Kazi vitakavyotumika kufanya tathmini ya uelekeo wa Sekta ya Nishati nchini.

Dkt. Biteko amewasisitiza Watumishi wote kutenda zaidi kuliko kusema, kujenga taasisi imara kuliko mtu imara na kujenga Sekta ya Nishati imara kuliko Waziri imara ili kuweza kuwahudumia wananchi vizuri na kwa haraka.

Aidha, ameagiza Watendaji kueleza mafanikio ya Sekta ya Nishati kwa watanzania ili wafahamu jinsi Rais Samia anavyojitoa katika kuiendeleza Sekta ya Nishati.

Vilevile, Dkt. Biteko ameagiza kufanyike tathmini ya Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa lengo la kufahamu mwelekeo wa utekelezaji wa mkakati huo na kuendelea kuboresha utekelezaji wake.

Katika kikao hicho cha Menejimenti ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake pia ilitolewa tathmini ya utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara iliyofanyika katika kipindi cha miezi mitatu kinachoishia mwezi Septemba 2024 ambapo Wakala wa Nishati Vijijini (REA) umeongoza kwa kufanya vizuri ukifuatiwa na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA).

Aidha, kwa tathmini ya utendaji kazi iliyofanyika ndani ya TANESCO, mikoa ya Kitanesco ya Singida, Kinondoni Kaskazini na Manyara imefanya vizuri zaidi katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Washindi wa tathmini hiyo ya utendaji kazi wamepatiwa zawadi ikiwemo barua za pongezi huku wale ambao hawakuvuka kiwango cha asilimia 80 wakitakiwa kuongeza juhudi.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba alisema kikao hicho ni mahsusi kwa ajili ya kufanya tathmini ya utendaji sekta ya Nishati kwa Wizara na Taasisi zake.

Taasisi zilizoshiriki kikao hicho ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC).

# KONGAMANO LA JOTOARDHI AFRIKA KULETA UWEKEZAJI NA UBUNIFU MPYA TANZANIA-KADUARA



Waziri wa Maji, Nishati na Madini wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Shaibu Kaduara akizungumza wakati wa hafla ya ufungaji wa Kongamano la Kimataifa la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) jijini Dar es Salaam tarehe 25 Oktoba, 2024.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio akizungumza wakati wa hafla ya ufungaji wa Kongamano la Kimataifa la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) jijini Dar es Salaam tarehe 25 Oktoba, 2024.

Waziri wa Maji, Nishati na Madini wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Shaibu Kaduara amesema Kongamano la Kimataifa la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) lililofanyika nchini kuanzia tarehe 21 Oktoba 2024 litaleta uwekezaji na ubunifu mpya katika uendelezaji wa nishati ya Jotoardhi.

Mhe. Kaduara amesema hayo wakati hafla ya ufungaji wa kongamano hilo iliyofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 25 Oktoba, 2024.

"Maarifa na utaalam uliopatikana katika kongamano hili utasaidia mustakabali wa Tanzania na Afrika katika kufikia suluhisho la upatikanaji wa nishati safi, kuongeza kasi ya maendeleo ya jotoardhi Tanzania na kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika uzalishaji umeme." Amesema Kaduara

Amesema Tanzania imepata heshima kubwa baada ya kuandaa kongamano hilo kwa mafanikio na imekuwa ni fursaya kutangaza maeneo yake yanayohitaji uendelezaji ikiwemo eneo la Ngozi mkoani Mbeya ambapo kunachimbwa visima vitatu vya uhakiki wa mashapo ya Jotoardhi.

Ameongeza kuwa, kwa kuandaa kongamano la ARGeo-C10 Tanzania imeonesha kwa vitendo nia yake ya kuendeleza jotoardhi, kushiriki katika biashara ya hewa ukaa na kutokuwa na uzalishaji wa hewa ya ukaa.

Mhe. Kaduara ametumia fursa ya kongamano hilo kuwasihi Washirika wa Maendeleo duniani kuendelea kuunga mkono jitihada za kukuza nishati ya Jotoardhi barani Afrika.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio, amesema Kongamano la ARGeo-C10 limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwani Nchi 14 ambazo ni Wanachama wa Shirikisho la Jotoardhi

Afrika zimeshiriki pamoja na nchi nyinginezo zipatazo 12.

Ameongeza kuwa Kongamano pia limehusisha Wataalam wabobezi kutoka mataifa hayo 26 ambao wametoa mafunzo maalum katika Jotoardhi ikiwemo masuala ya tathmini ya Jotoardhi na jinsi nishati hiyo itakavyosaidia kuangalia masoko ya hewa ya ukaa.

Amesema kupitia Kongamano hilo nchi nyingi zimeonesha nia ya kuwekeza Tanzania baada ya kuona utajiri wa jotoardhi uliopo na utayari wake katika kushirikiana na nchi nyingine duniani ili kuiendeleza.

Amesema nchi nyingi Afrika bado hazijatumia nishati hiyo ipasavyo hivyo Kongamano la ARGeo-C10 limelenga kuharakisha uendelezaji nishati ya Jotoardhi Afrika ili iwe na mchango mkubwa katika gridi za umeme kama ilivyo kwa vyanzo vingine kama vile maji.

Mwakilishi wa Spika la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt.Joseph Mhagama amesema kongamano hilo la Jotoardhi limewawezesha Wabunge walioshiriki kupata uelewa kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo matumizi ya moja kwa moja ya Jotoardhi,fursa, changamoto na biashara ya hewa ukaa hivyo uelewa huo utawasaidia kutoa ushauri kwa Serikali na kuisimamia Sekta ya Jotoardhi kwa ujumla.

Naye, Mkuu wa Ofisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Mazingira Duniani (UNEP) katika nchi za Kusini mwa Afrika, Meseret Teklemarian ameshukuru Serikali ya Tanzania kwa kuendesha kongamano la ARGeo-10 kwa mafanikio makubwa huku likipewa msukumo mkubwa na Serikali na kwamba UNEP itaendelea kuunga mkono Tanzania kwa namna mbalimbali ili kuendeleza nishati ya Jotoardhi.

Dkt. Peter Omenda, Rais wa Shirikisho la Jotoardhi Afrika (AGA), naye ameishukuru Tanzania kwa kuendesha kongamano hilo kwa mafaniko na kueleza kuwa ni kongamano bora linalopaswa kuigwa na nchi nyingine Afrika.

Ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kujitoa ipasavyo katika kuhakikisha kuwa Kongamano hilo linafanikiwa huku likiwa na washiriki wengi zaidi kuliko makongamano mengine yaliyopita.

Aidha ameeleza kuwa, Kongamano linalofuata litafanyika Comoro mwaka 2026.

Awali, Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mathew Mwangomba alisema ARGeo-C10 imeacha alama na kumbukumbu barani Afrika ambapo ameishukuru Serikali na wadau kwa kuwezesha kongamano hilo kufanyika kwa mafanikio.


Amesema Tanzania ipo tayari kushirikiana na wadau wengine ili kuendelea Jotoardhi kupitia utaalam na uwekezaji kwenye maeneo yenye mashapo ya Jotoardhi.




Waziri wa Maji, Nishati na Madini wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Shaibu Kaduara (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi ya Kongamano la Jotoardhi Afrika mara baada ya kufunga Kongamano hilo la Kimataifa la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) jijini Dar es Salaam tarehe 25 Oktoba, 2024. Kulia kwake ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Utawala na Sheria, Mhe. Joseph Mhagama na kushoto kwake ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt.James Mataragio.

# WATU MILIONI 300 AFRIKA KUTUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA IFIKAPO 2030- DKT. BITEKO

- Benki ya Dunia na AfDB zaunga mkono Ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia
- Mkutano wa Marais Afrika kufanyika Tanzania; Ajenda ya Nishati Safi kupewa kipaumbele
- Tanzania yawa mfano Afrika mapinduzi Sekta ya Nishati


Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt. Doto Biteko akizungumza wakati wa Kongamano na Jukwaa la Majadiliano kuhusu Masuala ya Nishati kwa Bara la Afrika( AEMP) kwa ngazi ya Mawaziri unaofanyika Jijini Dar es salaam.


Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akizungumza wakati wa Kongamano na Jukwaa la Majadiliano kuhusu Masuala ya Nishati kwa Bara la Afrika(AEMP) kwa ngazi ya Mawaziri unaofanyika Jijini Dar es salaam.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt. Doto Biteko amesema ifikapo mwaka 2030 watu milioni 300 katika Bara la Afrika watakuwa wanatumia Nishati Safi ya kupikia huku Tanzania ikiwa ni kinara katika kuhamasisha Ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia.

Amesema juhudi zinazofanyika katika kufikia lengo hilo zimepelekea Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Benki ya Dunia ( WB) kuunga mkono Ajenda ya Nishati Safi ya kupikia katika bara la Afrika. Biteko amesema hayo wakati akizungumza katika Mkutano wa Jukwaa la Majadiliano kuhusu Masuala ya Nishati kwa Bara la Afrika kwa ngazi ya Mawaziri unaofanyika Jijini Dar es salaam kwa siku mbili ulioandaliwa na Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na AfDB.

Amesema AfDB imeichangua Tanzania kufanya mkutano huo wa majadiliano kwa kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa kimaendeleo na mafanikio katika Sekta ya Nishati ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika zinazoshirikiana na benki hiyo na imekuwa mfano wa kuigwa na nchi hizo..

Ameeleza kuwa, katika mkutano huo masuala mbalimbali yanajadiliwa huku lengo kubwa likiwa ni kuweka mipango thabiti ya kuhakikisha kuwa watu Milioni 300 katika Bara la Afrika wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2030 ikiwa ni miaka 6 kutoka sasa. “ Mkutano huu pia ni sehemu ya maandalizi ya Mkutano wa Marais wa nchi za Afrika unaotarajiwa kufanyika mwaka 2025 ikiwa ni mwaliko wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye kinara wa ajenda ya Nishati safi ya kupikia Afrika.” Amesema Dkt. Biteko

Amesema Marais hao watakuja

nchini kujadili masuala ya nishati katika Bara la Afrika ikiwemo suala la watu milioni 300 Afrika kutumia nishati safi ya kupikia.

Ameongeza kuwa, mkutano huo utafanya tafakuri na utaweka mikakati ya kuhakikisha kuwa nishati safi ya kupikia inapatikana kwa uhakika na gharama nafuu ili kila mwananchi anaweza kuimudu.

Amesema mkutano huo ni muhimu kwa Tanzania hasa kwenye sekta ya nishati kwakuwa imefanya mapinduzi makubwa kwenye nishati na upatikanaji wa umeme nchini ni wa uhakika na miradi mikubwa inayotekelezwa ipo mwishoni na kwamba kazi kubwa iliyopo ni kuhakikisha watu wanapata umeme kila sehemu.

“Furaha yetu ni kwamba tumepata heshima kubwa ambayo haikuja hivihivi bali ni kutokana na mahusiano mazuri ya kidiplomasia kati nchi yetu, Benki ya Maendeleo ya Afrika ( AfDB) na Benki ya Dunia na kutokana pia na kupiga hatua katika masuala ya usimamizi mzuri wa kisera, uzalishaji, usafirishaji, usambazaji na upelekaji wa umeme vijijini.” Amesema Dkt. Biteko.

Amesema Tanzania imepiga hatua katika kupeleka umeme vijijini na ifikapo Desemba tutakuwa tumepeleka umeme katika vijiji vyote zaidi ya 12,000 na kuhamia katika vitongoji vyote.

Makamu wa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dkt. Kelvin Kairuki amesema Benki hiyo kwa kushirikiana na Benki ya Dunia itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kufanya kazi pamoja kwa sababu Tanzania iko katika mstari wa mbele katika kutekeleza Ajenda ya Nishati safi ya Kupikia ikilinganishwa na nchi nyingine zinazofanya kazi na benki hizo.

Amesema uamuzi wa kuamua mkutano mkubwa wa Marais ufanyike Tanzania ni pamoja na kumuunga mkono Rais Samia katika juhudi za utekelezaji wa Ajenda ya Nishati safi ya kupikia na kuwa kinara wa ajenda hiyo kwa nchi za Afrika.

Mkutano huo umehudhuriwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Kamishna wa Umeme na Nishari Jadidifu Mhandisi Inocent Luoga, Wakuu wa Taasisi zilizochini wa Wizara ya Nishati na wadau wa nishati kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya Tanzania.



Makamu wa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dkt. Kelvin Kairuki akizungumza wakati wa Kongamano na Jukwaa la Majadiliano kuhusu Masuala ya Nishati kwa Bara la Afrika(AEMP) kwa ngazi ya Mawaziri unaofanyika Jijini Dar es salaam.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt. Doto Biteko akiwa katika picha ya pamoja na Kamati ya Maandalizi ya Kongamano na Jukwaa la Majadiliano kuhusu Masuala ya Nishati kwa Bara la Afrika(AEMP) kwa ngazi ya Mawaziri unaofanyika Jijini Dar es salaam.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Dkt. James Andilile akizungumza wakati wa Kongamano na Jukwaa la Majadiliano kuhusu Masuala ya Nishati kwa Bara la Afrika(AEMP) kwa ngazi ya Mawaziri unaofanyika Jijini Dar es salaam.



Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Hassan Saidy (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mhandisi Gisima Nyamuhanga(kushoto) wakimsikiliza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko(hayupo pichani) akizungumza wakati wa Kongamano hilo

# KAMATI YA BUNGE YARIDHISHWA UTENDAJI KAZI WIZARA YA NISHATI

- Yakoshwa na ETDCO kuongeza ufanisi wa kazi
- Kapinga asema Serikali itaendelea kuboresha upatikanaji wa Nishati safi ya Kupikia



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga akijibu baadhi ya maswali yaliyoulizwa na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakati wa vikao vya kamati hiyo vinavyoendelea Bungeni Jijini Dodoma Tarehe 22 Oktoba, 2024.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeeleza kuridhishwa kwake na majukumu yanayotekelezwa na Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini yake katika kuiimarisha Sekta ya Nishati nchini.

Pongezi hizo zimetolewa baada ya Wizara ya Nishati kupitia Taasisi zake za Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Kampuni Tanzu ya TANESCO ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme (ETDCO) kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa majukumu yake kwa Kamati hiyo.

"Naipongeza Serikali kwa namna ambavyo imejipanga katika kusimamia Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia ili lengo la asilimia 80 la Watanzania kutumia Nishati Safi ya Kupikia ifikapo 2034 liweze kufikiwa." Amesema Mhe. Mathayo

Aidha, amempongeza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Biteko kwa usimamizi wa Kampuni ya ETDCO ambayo inaendelea kutekeleza mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Tabora hadi Katavi ambao umefikia asilimia 80 na utakapokamilika utawezesha Mkoa wa Katavi kuunganishwa na gridi ya Taifa.

Mradi mwingine unaotekelezwa na ETDCO ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka

Tabora hadi wilayani Urambo ambao umefikia asilimia 80 na unatarajiwa kuimarisha upatikanaji wa huduma ya umeme Urambo na maeneo ya jirani.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga amewashukuru wajumbe wa Kamati hiyo kwa michango yao katika kuboresha sekta ya nishati nchini.

" Kuimarika kwa Kampuni hii ya ETDCO ni jitihada za kiongozi wetu Mhe. Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati katika kuiongezea ufanisi, kampuni hii ili iweze kufanya vizuri." Amesema Mhe.Kapinga

Ameongeza kuwa Wizara ya nishati itaongeza nguvu katika kusimamia miradi ya umeme ili ikamilike kwa wakati.

Akiongelea kuhusu Nishati Safi ya kupikia, Mhe. Kapinga amesema Serikali itaendelea kuboresha upatikanaji wa nishati hiyo na kuongeza kuwa, mbali ya majiko ya gesi kuna majiko ya umeme ambayo yanatumia umeme kidogo na kwamba kinachohitajika sasa ni suala la jamii kubadili fikra.

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba amesema Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia ni wa miaka kumi na hivi sasa upo hatua za awali za utekelezaji wake.

"Mkakati huu umezinduliwa mwezi wa sita mwaka huu, vitu vingi vipo kwenye hatua za mwanzo tunaendelea na mazungumzo na Mawakala ili kufunga mita kwenye mitungi ya gesi." Amesema Mha. Mramba



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba akieleza Mikakati ya Nishati Safi ya Kupikia kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakati wa vikao vya kamati hiyo vinavyoendelea Bungeni Jijini Dodoma Tarehe 22 Oktoba, 2024.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mhe. David Mathayo. Akiipongeza Wizara ya Nishati kwa namna ambavyo imejipanga katika kusimamia Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia wakati wa vikao vya kamati hiyo vinavyoendelea Bungeni Jijini Dodoma Tarehe 22 Oktoba, 2024.

# TANZANIA NA SINGAPORE KUIMARISHA UHUSIANO WAKE

- Tanzania na Singapore Kuongeza Kiwango cha Ufanyaji Biashara



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk Doto Biteko akizungumza na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Viwanda na Biashara wa Singapore Mhe. Gan Kim Yong, nchini Singapore tarehe 21 Oktoba, 2024.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa uhusiano wa Tanzania na Singapore ni wa muda mrefu na kuwa nchi hizo zinatakiwa kuangalia sababu za uwepo wa uhusiano huo na kuongeza kiwango cha ufanyaji biashara kati yake.

Dkt. Biteko ameyasema hayo Oktoba 21, 2024 akiwa nchini Singapore mara baada ya kukutana na kufanya mazungunzo na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Viwanda na Biashara wa Singapore Mhe. Gan Kim Yong.

“ Tunatakiwa kujifunza kutokana na uhusiano huu na hasa kutoka Singapore kwa kuwa mmepiga hatua katika sekta ya nishati hadi kuwa na uwezo wa kufikia mahitaji ya juu ya umeme ya zaidi ya Gigawati 8, hicho ni kiasi kikubwa ikilinganishwa na Tanzania yenye takribani Megawati 3000 ambapo hadi mwaka 2030 tumepanga kufikia Megawati 10,000," amesema Dkt. Biteko.

Amesisitiza “ Mpango huo hauwezi kutokea bila kuwa na ushirikiano na wadau na nchi zingine kama Singapore, ni matumaini yetu kuona ushirikiano huu unaendelea kukua kati ya nchi zetu na kuleta manufaa kwa wananchi”

Dkt. Biteko ameipongeza Singapore kwa uzalishaji wa umeme wa jua na kusema kuwa Tanzania inaendelea na jitihada zake za kuzalisha umeme huo.

Akitaja miradi ya nishati inayoendelea kutekelezwa, Dkt. Biteko amesema kuwa kwa sasa nchi inaendelea na utekelezaji wa mradi mkubwa utakaozalisha megawati 2115. Aidha, upembuzi yakinifu unaendelea kuhusu miradi mbalimbali ya uzalishaji umeme.

Fauka ya hayo, Dkt. Biteko amemualika Naibu Waziri Mkuu wa Singapore, Mhe. Yong nchini Tanzania. “Kwa niaba ya Serikali na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tutafurahi ukija Tanzania na tuna amini kuna maeneo mengi ya kushirikiana nanyi," amesema Dkt. Biteko.

Naye, Naibu Waziri Mkuu wa Singapore, Mhe. Yong amesema kuwa nchi yake ipo tayari kuendelea kushirikiana na Tanzania na kuwa nchi hizo zina mahitaji ya kufanana.

Aidha, amesema kuwa Singapore inategemea zaidi gesi asilia licha ya kutumia pia umeme unaozalishwa kwa maji, jua na upepo. Vilevile nchi yake iko tayari kushirikiana na Tanzania katika kubadilishana uzoefu wa masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya nishati.

# DKT. BITEKO AFANYA MAZUNGUMZO NA MWAKILISHI WA HESHIMA WA TANZANIA SINGAPORE



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, akizungumza na Mwakilishi wa Heshima wa Tanzania nchini Singapore, Bw. Teo Siong Seng, tarehe 21 Oktoba 2024.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko Oktoba 21, 2024 akiwa nchini Singapore amekutana na kufanya mazungunzo na Mwakilishi wa Heshima wa Tanzania nchini humo, Bw. Teo Siong Seng ambaye pia ni mwenyekiti mwenza wa Kampuni ya Pacific International Lines (Pte) Ltd.

Katika mazungumzo yao, Dkt. Biteko amesema kuwa Serikali inathamini kazi ya uwakilishi inayofanywa na Bw. Seng na kuwa itaendelea kumpa ushirikiano katika kutekeleza jukumu hilo.

Pia, ameikaribisha sekta binafsi kwa ajili ya kuwekeza katika sekta ya nishati ili kuongeza kasi ya uzalishaji, uunganishaji na usambazaji wa nishati nchini Tanzania.

Kwa upande wake, Bw. Seng ameishukuru Serikali kwa kumpa fursa hiyo ya kuiwakilisha Tanzania nchini Singapore huku akiahidi kuendelea na jukumu hilo ikiwa ni pamoja kutangaza utalii.

Dkt. Biteko yuko nchini Singapore kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa 17 wa Wiki ya Kimataifa ya Nishati ambao unalenga kuwakutanisha wadau wa sekta hiyo kwa ajili ya kujadili mahitaji ya nishati yanayoongezeka duniani ikiwa ni pamoja na kuharakisha juhudi za kupunguza hewa ya ukaa.

# KONGAMANO LA KIMATAIFA LA JOTOARDHI LAANZA KWA MAFANIKIO DAR ES SALAAM

- Lahusisha nchi 21 na Washiriki 800
- Kuangazia Sera, fursa za masoko na uwekezaji
- Kamishna Luoga asema lengo ni kuendeleza nishati ya Jotoardhi nchini
- UNEP yaipongeza Tanzania kwa maandalizi




Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga akifungua mafunzo kuhusu masuala mbalimbali ya Jotoardhi kwa niaba ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt.Khatibu Kazungu ikiwa ni sehemu ya programu ya siku saba Katika Kongamano la Kimataifa la Jotoardhi linaloendelea jijini Dar es Salaam.

Kongamano la 10 la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) limeanza kwa mafanikio jijini Dar es Salaam ambapo Wataalam takriban 800 kutoka 21 duniani wameshiriki.

Hayo yameelezwa na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga wakati akifungua mafunzo kuhusu masuala mbalimbali ya Jotoardhi kwa niaba ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. Khatibu Kazungu ikiwa ni sehemu ya programu ya siku saba za Kongamano hilo.

"Katika Kongamano hili washiriki watafaidika na masuala mbalimbali ikiwemo kupata ufahamu wa kina kuhusu maendeleo ya rasilimali za jotoardhi kupitia mazungumzo na warsha za kiufundi, Kubadilishana uzoefu, kutembelea na kujifunza kwa vitendo katika maeneo ya miradi ya jotoardhi, kujadili athari za masoko ya kaboni (carbon markets) na kukuza Uwezo: Kupitia kozi fupi za kiufundi (Pannel and Parallel Sessions." Amesema Mhandisi Luoga

Ameongeza kuwa, kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa kongamano hilo kunatokana na juhudi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uendelezaji wa Sekta ya Nishati ikiwemo Jotoardhi.

" Ili tuweze kuwa na umeme wa uhakika na usalama wa nishati nchini lazima umeme uzalishwe kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo Maji, Gesi, Jua, Upepo na Jotoardhi yenyewe na lengo la Serikali ni kuachana na utegemezi vyanzo vichache vya umeme." Amesema Mhandisi Luoga

Ameeleza kuwa, Kongamano hilo la Kimataifa la Jotoardhi linaamsha ari mpya katika uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania kwani litasaidia pia kuongeza fursa za uwekezaji kwenye sekta hiyo.

Kongamano litafunguliwa na Makamu wa Rais, Mhe.Dkt. Philip Isdor Mpango ambapo nchi mbalimbali duniani zinazoshirikiana na Tanzania katika kuendeleza rasilimali ya Jotoardhi zinashiriki.

Ametanabaisha kuwa, Tanzania ina maeneo takriban 52 yaliyoainishwa kwa

ajili ya uendelezaji wa nishati ya Jotoardhi ambapo maeneo matano tayari yanaendelezwa, ikiwemo Ngozi, Kiejo-Mbaka, Ruhoi, Natron na Songwe.

Kwa upande wake, Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mathew Mwangomba amesema Kongamano hilo linahusisha wadau mbalimbali duniani ikiwemo watalam wa jotoardhi ambapo kongamano litaangazia masuala mbalimbali ikiwemo masoko ya gesi ya ukaa na upunguzaji wa gesi ya ukaa.

Ametaja Kauli mbiu ya Kongamano hilo kuwa ni, Kuharakisha Maendeleo ya Rasilimali za Jotoardhi katika Afrika, Masoko ya Gesi ya Ukaa na Upiunguzaji wa Gesi ya Ukaa".

Ametaja faida za ARGeo C-10 kuwa ni pamoja na kufungua fursa zinazotokana na jotoardhi na kuharakisha maendeleo ya nishati hiyo Tazania hali itakayoongeza pia pato la Taifa na kuongeza kiasi cha umeme.

Amesema katika Kongamano lililofanyika mwaka 2014 ambapo Tanzania ilikuwa nchi mwenyeji, lilileta matokeo chanya ikiwemo uanzishwaji wa kampuni ya Jotoardhi Tanzania, Wataalam wa Kitanzania kupata mafunzo nje ya nchi na kuongeza mchango wa wadau wa maendeleo katika Jotoardhi ikiwemo Japan (JICA), Iceland, New Zealand na Marekani.

Naye, Mkuu wa Ofisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maziringira (UNEP) katika nchi za Kusini mwa Afrika, Meseret Teklemarian ameipongeza Tanzania kwa kuandaa Kongamano hilo kwa mafanikio makubwa.

Pia ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kulipa umuhimu mkubwa Kongamano hilo kwani maandalizi ya Kongamano husika yameshirikisha Watalam kutoka Sekta mbalimbali huku Watalam wengi kutoka Taasisi mbalimbali na mashirika binafsi wakihudhuria mafunzo yanayoendelea katka kongamano hilo.






Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga (katikati waliokaa) akifungua mafunzo kuhusu masuala mbalimbali ya Jotoardhi kwa niaba ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. Khatibu Kazungu ikiwa ni sehemu ya programu ya siku saba Katika Kongamano la Kimataifa la Jotoardhi linaloendelea jijini Dar es Salaam. Wa pili kulia ni Mkuu wa Ofisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maziringira (UNEP) katika nchi za Kusini mwa Afrika, Meseret Teklemarian.

# DKT.MATARAGIO AKARIBISHA UWEKEZAJI VITALU VYA MAFUTA NA GESI ASILIA

- Ni Eyasi-Wembere, Songo songo Magharibi na Mnazi Bay
- Jotoardhi nayo yatajwa Kongamano la Mafuta Afrika
- Kamishna Shirima atoa uhakika wa miundombinu ya gesi asilia Tanzania




Naibu Katibu Mkuu Dkt. James Mataragio akiwakaribisha wawekezaji wakati akitoa wasilisho la sekta ya mafuta na gesi Tanzani katika Kongamano la Wiki ya Mafuta (Afrika Oil Week 2024) lililofanyika Nchini Afrika Kusini, Tarehe 10 Oktoba 2024.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Dkt. James Mataragio amewakaribisha wawekezaji kuingia ubia na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa ajili ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini.

Dkt. Mataragio amewakaribisha wawekezaji wakati akitoa wasilisho la sekta ya mafuta na gesi Tanzani katika Kongamano la Wiki ya Mafuta (Afrika Oil Week 2024) lililofanyika Nchini Afrika Kusini, Tarehe 10 Oktoba 2024.

Amevitaja vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kuwa ni Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi - Wembere, Songo Songo Magharibi, 41B na 41C na hii ni kutokana na taarifa zilizofanyiwa utafiti zinazoonesha viashiria vya uwepo wa rasimlimali hizo katika maeneo hayo.

Pia amekaribisha uwekezaji katika miradi ya kuzalisha umeme wa jotoardhi katika maeneo ya Ngozi, Kiejo-Mbaka, Songwe, Luhoi na Natron.

Dkt. Mataragio amesema Tanzania ni sehemu ya kuwekeza kutokana na utulivu wa kisiasa, mazingira rafiki ya uwekezaji, miundombinu wezeshi, uwepo wa soko la ndani na soko katika nchi jirani.

Vilevile, Dkt. Mataragio ameeleza jinsi Tanzania inavyotekeleza miradi mbalimbali mikubwa ya umeme ikiwemo mradi wa Julius Nyerere (JNHPP) ambayo

inaiwezesha Tanzania kuwa na umeme wa kutosheleza mahitaji ya nchi na mwingine utauzwa katika nchi jirani.

Pia ameeleza kuhusu utekelezaji wa mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (EACOP) ambapo Serikali ina hisa za asilimia 15 na mradi wa Gesi Asilia iliyosindikwa ( LNG) ambao majadiliano yake yanaendelea.

Kwa upande wake, Kamishna wa Petroli na Gesi, Godluck Shirima wakati akishiriki katika mjadala wa kitaalam kuhusu uchumi wa gesi alieleza kuhusu miundombinu ya usafirishaji wa gesi iliyopo nchini ikiwa ni pamoja na bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam na mikakati ya Serikali ya kupeleka gesi katika nchi za jirani ikiwemo Kenya, Uganda na Malawi.

Aidha, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Mha. Charles Sangweni alieleza kuhusu mpango wa Tanzania kutangaza duru ya tano ya vitalu 24 vya gesi asilia ambapo vitalu 21 vipo katika kina kirefu cha bahari ya hindi na vitalu 3 vipo katika ziwa Tanganyika.

Alieleza kuwa, vitalu vyote vina data za kutosha ambazo zinaashiria uwepo wa rasilimali za mafuta na gesi asilia hivyo aliwakaribisha wawekezaji katika mkondo wa juu kuchangamkia fursa hiyo.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Mha. Charles Sangweni akieleza kuhusu mpango wa Tanzania kutangaza duru ya tano ya vitalu 24 vya gesi asilia wakati wa Kongamano la Wiki ya Mafuta (Afrika Oil Week 2024) lililofanyika Nchini Afrika Kusini, Tarehe 10 Oktoba 2024



Kamishna wa Petroli na Gesi, Godluck Shirima (Kulia) akishiriki katika mjadala wa kitaalam kuhusu uchumi wa gesi, alieleza kuhusu miundombinu ya usafirishaji wa gesi iliyopo nchini ikiwa ni pamoja na bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam wakati wa Kongamano la Wiki ya Mafuta (Afrika Oil Week 2024) lililofanyika Nchini Afrika Kusini, Tarehe 10 Oktoba 2024.

# SERIKALI ITAENDELEA KUSHIRIKISHA WAWEKEZAJI UENDELEZAJI NISHATI JADIDIFU- DKT.MATARAGIO

- Asema maeneo yenye vyanzo vya Nishati Jadidifu yameshatambuliwa
- Mikoa 16 yatajwa kuwa na rasilimali ya Jotoardh



Naibu Katibu Mkuu Dkt. James Mataragio akizungumza wakati wa kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kilichofanyika Bungeni Jijini Dodoma Tarehe 23 Oktoba, 2024.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio amesema Serikali itaendelea kuwashirikisha wawekezaji katika maeneo yenye nishati jadidifu ili kuyaendeleza na hivyo kuwezesha azma ya nchi kuwa na umeme unaotokana na vyanzo mchanganyiko.

Amesema hayo jijini Dodoma wakati Wizara ya Nishati ikiwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi ya Nishati Jadidifu inayotokana na Jotoardhi, Upepo na Jua kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

"Tumeshayatambua maeneo ambayo nishati jadidifu inapatikana, kwa upande wa Jotoardhi tunaendelea na uhakiki wa rasilimali hiyo ambayo inahusisha uchorongaji wa visima." Amesema Dkt. Mataragio

Dkt. Mataragio amesema Nishati Jadidifu kama Jotoardhi, Jua na Upepo ni miongoni mwa nishati safi ambazo zinaendana na malengo ya dunia ya kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi Gissima Nyamo-Hanga alisema rasilimali ya Jotoardhi ni jadidifu na endelevu na inatumika kwa kuzalisha umeme na matumizi mengine.

"Tanzania inakadiriwa kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa jotoardhi usiopungua megawati 5,000 kutoka katika vyanzo 52 vinavyopatikana ndani ya mikoa

16 nchini." Alisema Mhandisi Nyamo-Hanga

Akielezea hatua za utekelezaji wa miradi hiyo Mhandisi Nyamo-Hanga alisema mradi wa Ngozi uliopo mkoani Mbeya upo katika hatua ya uhakiki wa rasilimali jotoardhi ambayo inahusisha uchorongaji wa visima vya uhakiki.

Alisema Mradi huo ukikamilika utazalisha megawati 70 ambapo utaanza na megawati 30.

Mradi mwingine ni Kiejo-Mbaka ambao upo wilayani Rungwe Mkoa wa Mbeya ambao umefikia hatua ya uhakiki wa rasilimali ya joto ardhi ikihusisha uchorongaji wa visima virefu vya utafiti.

Alisema mradi huo utazalisha Megawati 60 ambapo utaanza na megawati 10.

Aliongeza kuwa, Mradi wa Songwe upo katika hatua ya uchorongaji wa visima vinne vya uhakiki wa rasilimali.

Akieleza kuhusu utekelezaji wa miradi ya umeme jua, Mhandisi Nyamo-Hanga alisema utafiti unaonesha maeneo mengi nchini yanaweza kufungwa mitambo ya umeme jua ikiwemo Dodoma, Singida, Tabora, Arusha, Shinyanga na Iringa.

Alisema mradi wa umeme jua ambao upo katika hatua ya utekelezaji ni wa megawati 150 uliopo Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga ambao unatekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza itazalisha megawati 50 na awamu ya pili megawati 100.

Alisema miradi ya upepo ipo katika hatua ya upembuzi yakinifu na itakapokamilika itaongeza kiwango cha umeme kinachotokana na na nishati jadidifu.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mhe. David Mathayo akizungumza wakati wa kikao cha kamati hiyo Bungeni Jijini Dodoma Tarehe 23 Oktoba, 2024.



Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi Gissima Nyamo-Hanga akiwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi ya Nishati Jadidifu inayotokana na Jotoardhi, Upepo na Jua kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. wakati wa kikao cha kamati hiyo kilichofanyika Bungeni Jijini Dodoma Tarehe 23 Oktoba, 2024.

# TUNAIMARISHA MAZINGIRA YA UWEKEZAJI NA MIUNDOMBINU YA NISHATI ILIKUFIKISHA HUDUMA KWA WOTE- DKT.MATARAGIO

- Asisitiza nia ya Serikali ni kutoa huduma stahiki bila kuangalia umbali au kipato
- Apongeza kampuni ya Puma Energy Tanzania kushirikiana na Serikali uhamasishaji Nishati Safi ya Kupikia



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio akizungumza jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya utoaji Tuzo kwa Mawakala na Wadau wa Kampuni ya Puma Energy Tanzania ambayo inaunga mkono juhudi za Serikali za kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kupitia bidhaa za Puma Gas.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio amesema Serikali inaendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji na miundombinu ya Sekta ya Nishati nchini ili kuwezesha wananchi kufikiwa na huduma stahiki bila kujali umbali na vipato vyao.

Dkt. Mataragio ameyaeleza hayo jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya utoaji Tuzo kwa Mawakala na Wadau wa Kampuni ya Puma Energy Tanzania ambayo inaunga mkono juhudi za Serikali za kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kupitia bidhaa za Puma Gas.

Dkt. Mataragio amesema moja ya majukumu ya Wizara ya Nishati ni kukutana na wadau mbalimbali wakiwemo watoa huduma na watumiaji ili kuimarisha ushirikiano kati ya sekta binafsi na Serikali utakaopelekea utoaji wa huduma bora kwa wananchi ikiwa ni moja ya vipaumbele vya Serikali.

Katika hafla hiyo, Dkt.Mataragio ameipongeza kampuni ya Puma kwa jitihada zinazounga mkono juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuhamasisha jamii ili itumie Nishati Safi ya Kupikia na hivyo kutimiza lengo la asilimia 80 ya Watanzania kutumia Nishati Safi ya Kupikia ifikapo mwaka 2034.

Amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.

Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa Balozi na kinara katika kuhamasisha matumizi ya Nshati Safi ya Kupikia nchini na Duniani ili kuhakikisha Watu wanaondokana na matumizi ya kuni na mkaa ambao una madhara kwa afya na kusababisha uharibifu wa mazingira.

Kuhusu Tuzo hizo zilizotolewa na Puma Energy Tanzania kwa Mawakala na Wadau mbalimbali nchini, Dkt.Mataragio ameelekeza kuwa ziwe chachu ya kuendelea kufanya kazi kwa weledi na ufanisi kulingana na vigezo na masharriti ya Kampuni kwa maslahi ya jamii.

Amesema kupitia mfano uliooneshwa na Puma Energy Tanzania wa kuwakutanisha wadau wake kila mwaka ili kuzungumzia mafanikio na changamoto zilizopatikana, iwe ni chachu kwa kampuni nyingine kuiga mfano huo ambao unasaidia kukuza sekta ya Nishati nchini.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Puma EnergyTanzania, Bi. Fatma Abdallah ameishukuru Serikali kwa hatua mbalimbali

za kuhamasisha matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia na kuahidi kuendelea kuunga mkono juhudi hizo kwa kuwafikishia wananchi bidhaa ya Puma Gas kupitia kwa Mawakala na Wadau waliopo maeneo mbalimbali.

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na Kamishna wa Petroli na Gesi, Godluck Shirima.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio (katikati), akiwa na Kamishna wa Petroli na Gesi, Godluck Shirika pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Puma Energy Tanzania, Bi. Fatma Abdallah jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya utoaji Tuzo kwa Mawakala na Wadau wa Kampuni ya Puma Energy Tanzania ambayo inaunga mkono juhudi za Serikali za kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kupitia bidhaa za Puma Gas.

# SERIKALI KUJA NA MKAKATI WA MAWASILIANO WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA- KAMISHNA LUOGA

- Lengo ni kutoa elimu na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia
- Ni nyenzo  muhimu katika safari ya matumizi ya nishati safi ya kupikia



Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga wakati akichangia mada katika Mjadala Jukwaa la Majadiliano kuhusu Masuala ya Nishati kwa Bara la Afrika uliondaliwa na Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), uliofanyika tarehe 16 na 17 Oktoba, 2024.

Imeelezwa kuwa Tanzania ipo katika hatua ya maandalizi ya Mkakati wa Mawasiliano wa Nishati Safi ya Kupikia wenye lengo la kutoa elimu na kuhamasisha matumizi ya Nishati safi ya kupikia nchini.

Hayo yametanabaishwa na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga wakati akichangia mada katika Mjadala Jukwaa la Majadiliano kuhusu Masuala ya Nishati kwa Bara la Afrika uliondaliwa na Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), uliofanyika tarehe 16 na 17 Oktoba, 2024.

Kongamano hilo lilihusisha Serikali, Washirika wa Maendeleo, Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi ambpo Mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe.Dkt. Doto Biteko.

Luoga amesema mkakati huo utawezesha utoaji wa elimu ya nishati hiyo kwa makundi yote ya wananchi nchini.

Ameongeza kuwa mkakati huo ndiyo utakuwa nyenzo na silaha muhimu ya kuweza kufikia azma ya Serikali ya kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya watanzania watakuwa wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.

" Tulipoanza safari ya matumizi ya nishati safi ya Kupikia Mwaka 2022 tulikuwa na asilimia isiyozidi 10 ya kaya zinazotumia nishati safi lakini kiasi hiki kitakuwa kimeongezeka sana kutokana na juhudi zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kuhamasisha matumizi ya teknolojia za nishati safi." Amesema Kamishna Luoga

Mwezi Mei, 2024 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ni kinara wa Ajenda ya Matumizi ya Nishati ya Kupikia alizindua Mkakati wa Miaka 10 wa Kitaifa wa Nishati safi ya Kupikia ambao umeelekeza kuwa asilimia 80 ya watanzania wote wawe wamehamia katika matumizi ya Nishati safi ya Kupikia ifikapo mwaka 2034.

Viongozi wengine walioshiriki Kongamano hilo ni Mha.Felchesmi Mramba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt Kevin Kariuki, Makamu wa Rais wa AfDB na Wakuu wa Taasisi za TANESCO, REA, TPDC na EWURA.

# WATAALAMU WA MAABARA TOENI MAJIBU SAHIHI KUWASAIDIA WATANZANIA - DKT. BITEKO

- Serikali Yafanya Mageuzi Makubwa Sekta ya Afya Nchini
- Wataalam wa Maabara za Binadamu Wasisitizwa Kulinda Taaluma Yao
- Tanzania ya Tatu Barani Afrika kwa Huduma Bora za Maabara



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk Doto Biteko akizungumza katika ufunguzi wa Kongamano la 37 la Kisayansi la Wataalamu wa Maabara za Afya nchini na Kongamano la 23 la Kisayansi la HUOQAS na Mkutano Mkuu wa Mwaka, jijini Dodoma tarehe 2 Oktoba , 2024.

Naibu Waziri Mkuu wa Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ametoa wito kwa Wataalam wa Maabara za binadamu nchini kuionea wivu taaluma yao kwa kuwa ina mchango mkubwa katika utoaji wa huduma za afya kwa Watanzania.

Dkt. Biteko amesema hayo Oktoba 2, 2024 Jijini Dodoma wakati akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika ufunguzi wa Kongamano la 37 la Kisayansi la Wataalamu wa Maabara za Afya nchini na Kongamano la 23 la Kisayansi la HUOQAS na Mkutano Mkuu wa Mwaka.

“ Wito wangu kwenu ioneeni wivu, muipende na kuithamini taaluma yenu, msikae pembeni mnapoona kuna changamoto semeni bila kuogopa. Wataalamu wa Maabara bila ninyi tiba haiwezi kufanyika na mfanye kila mtu awaheshimu,” amesema Dkt. Biteko.

Dkt. Biteko amesisitiza “ Nataka niwaambie mnapofanya kazi hii mnawahudumia Watanzania tufanye kwa upendo na tuwape majibu sahihi ili kuisaidia Serikali yetu kuwa mhudumu wa kweli wa wananchi.”

Aidha, Dkt. Biteko ameelekeza waajiri nchini kuruhusu watumishi wao wa kada ya maabara kushiriki katika makongamano ya kitaaluma huku akiwataka washiriki kujifunza kupitia mada zitakazowasilishwa na baadaye kuwashirikisha wataalam wenzao ambao hawakuhudhuria.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko

amesema kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya itafanyia kazi changamoto zote zilizowasiliahwa na MeLSET.

" Changamoto zote nimezichukua na naitaka Wizara kuchukua hotuba ya MeLSAT na kuzifanyia kazi changamoto zote zilizowasilishwa katika mkutano ili mwaka ujao changamoto zisiwe hizi tuwe na masuala mengine ya kuzungumza," ameeleza Dkt. Biteko.

Naye, Waziri wa Afya, Mhe. Jenista Mhagama amesema kuwa Serikali imefanya maboresho makubwa kwenye sekta ya afya na hiyo inaonesha hatua kubwa imepigwa huku akitaja shilingi trilioni 1.2 zilizotumika kuboresha maabara za afya nchini.

Ametaja eneo lingine lililoboreshwa katika sekta hiyo ni vitendea kazi vya kiuchunguzi kwa uwepo wa vifaa vya kisasa zikiwemo mashine 13 za MRI Digital xray 346, ulta sound 476 na ufundishaji wa ubingwa bobezi.

" Maboresho hayo yamegusa pia Mfuko wa ufadhili wa Rais Samia ambapo kwa kipindi cha miaka mitatu pekee umeshagharamia kiasi shilingi bilioni 9 ili kusomesha wataalamu wa sekta ya afya hapa nchini. Tumetanua wigo wa utalii wa afya kupitia uwekezaji huu uliofanywa na Mhe. Rais Samia." A mesisitiza Mhe. Mhagama.

Kaimu Mganda Mkuu wa Serikali, Dkt. Saitore Laizer amesema kuwa Wizara ya Afya imekuwa mstari wa mbele kukuza vyama mbalimbali vya kitaaluma ili viweze kusaidia kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali yanayolenga kuimarisha sekta ya afya nchini.

Amebainisha kuwa baada ya Serikali kuwekeza katika vifaa tiba na miundombinu pamoja na watumishi suala kubwa ni kuhakikisha kuna ubora wa huduma za afya na kuwa hicho ni kipaumbele ili mambo yote yaliyofanyika yaweze kuwa na tija.

" Suala la usugu wa vimelea vinaweza kuhama kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kama yalivyo magonjwa na ikifika huko maana yake tunaweza kupoteza maisha na gharama kubwa. Aidha, hakuna huduma bora za tiba bila ya huduma bora za uchunguzi na ndio maana kuanzia mwaka jana Serikali imeanza kutoa ufadhili wa masomi kwa kusomesha wataalamu wa maabara katika ngazi za kati katika vyuo vya umma, binafsi na mashirika ya dini hii inaonesha dhamira ya Serikali katika kuendelea kuimarisha sekta hii muhimu." Amesema Dkt. Laizer.

Rais wa Chama Cha Wataalam wa Maabara za Afya Tanzania (MeLSAT), Bw. Yahya Mnung'a amesema kuwa lengo la Kongamano hilo ni kuwakutanisha wataalam na kutatua changamoto za kitaaluma katika maabara za binaadamu pamoja na uwepo wa maonesho ya vifaa vinavyotumika katika maabara za binadamu.

Ameongeza kuwa MeLSAT inaendelea kuimarisha ushirikiano na vyama vya kitaaluma nchini pamoja na nje ya nchi na kuwa Tanzania.

" Maabara ya Afya ya Jamii ya Tanzania imekuwa ikifanya kazi nzuri na maabara yetu ni kati ya Maabara tatu bora barani Afrika. Tunaiomba Serikali iridhie ombi letu la kupandisha hadhi maabara hii ili kuwa Taasisi kwa kuwa inafanyakazi kubwa ndani na nje ya nchi," amesema Bw. Mnung'a.

Ameongeza kuwa wataalamu hao wataendelea kutoa huduma kwa Watanzania licha ya uwepo wao kwa idadi ndogo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Shirikisho la Wataalamu wa Maabara za Afya Afrika (FeLPA), Bw. Mulate Mubanga amesema kuwa idadi kubwa ya watu hupata madhara kwa kutumia dawa bila kufanya vipomo vya maabara na kuwa ni vyema Serikali barani Afrika pamoja na wadau wa sekta hiyo kupatia ufumbuzi changamoto hiyo.

" Naipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuwa na idadi kubwa ya maabara pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanya katika maabara, aidha elimu kuhusu matumizi ya dawa itolewe kwa wananchi ili kupunguza usugu wa dawa . Tunatumaini Serikali na wadau itaendelea kutoa elimu ya matumizi ya dawa kwa faida ya kizazi kijacho. Amesema Bw. Mubanga.

# MRAMBA AKAGUA JENGO LA WIZARA YA NISHATI MTUMBA

- Asisitiza utekelezaji wa agizo la Dkt.Biteko la ufungaji mitambo ya umeme Jua
- Jengo lafikia asilimia 84.3


Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (wa nne kushoto) pamoja na Menejimenti ya Wizara ya Nishati wakimsikiliza Msimamizi wa ujenzi wa jengo la Wizara ya Nishati, Alphonce Kilovele (wa kwanza kushoto) wakati wa ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa jengo hilo katika Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma.


Muonekano wa jengo la Wizara ya Nishati lililopo katika Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba leo ameongoza Menejimenti ya Wizara ya Nishati kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la Wizara hiyo katika Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma.

Akiwa katika jengo hilo alielezwa na Msimamizi wa ujenzi wa jengo kutoka Wizara ya Nishati, Alphonce Kilovele kuwa, ujenzi umefikia asilimia 84.3 na kwamba ifikapo mwezi Januari 2025 litakuwa tayari kwa matumizi.

Kilovele ameieleza Menejimenti ya Wizara ya Nishati kuwa, kazi zinazoendelea sasa ni za umaliziaji wa huduma saidizi ikiwemo miundombinu ya umeme, maji, zimamoto, Tehama, viyoyozi na vioo.

Ameeleza kuwa, jengo hilo litakalochukua watumishi 200 hadi 300 linafungwa mifumo ya umeme inayozingatia matumizi bora ya Nishati (energy efficiency) ikizingatiwa kuwa Wizara ya Nishati ni kinara wa usimamizi wa matumizi bora ya nishati nchini.

Katika ziara hiyo, Mhandisi Mramba amewakumbusha wasimamizi wa jengo hilo kuhakikisha kuwa agizo la Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko la majengo yote ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kufungwa mifumo ya nishati jadidifu ikiwemo umeme Jua linazingatiwa.

# WIZARA YA NISHATI NA UNDP ZAWANOA WATAALAM MATUMIZI BORA YA NISHATI

- Ni Taasisi zinazosimamia Matumizi Bora na Sahihi ya Nishati nchini
- Wataalam kuja na andiko la kusimamia ubora wa bidhaa za Nishati
- UNDP yaahidi kuendeleza ushirikiano matumizi sahihi ya Nishati



Kaimu Kamishna Msaidizi wa Nishati Jadidifu kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Imani Mruma, akizungumza na Wadau wakati wa Warsha ya Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Matumizi bora ya Nishati Tanzania inayofanyika tarehe 1 hadi 3 Oktoba, Mkoani Morogoro.

Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) wameandaa warsha itakayowawezesha Wataalam kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali kupitia nyaraka zitakazowezesha kuandaa vigezo vya kitaalam vitakavyoongoza kazi ya usimamizi na ukaguzi wa matumizi bora ya nishati nchini.

Warsha hiyo imehusisha wadau mbalimbali ikiwemo Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Pia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi( VETA), Taasisi ya Elimu ya Juu Tanzania(TCU) na Baraza la Taifa la Elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (NACTVET).

Akizungumza katika warsha hiyo mkoani Morogoro, Oktoba 2, 2024, Kaimu Kamishna Msaidizi wa Nishati Jadidifu kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Imani Mruma, amesema warsha hiyo imezilenga zaidi Taasisi zinazosimamia matumizi bora na sahihi ya nishati nchini.

Amesema baada ya warsha hiyo, wadau hao kwa pamoja watatoa andiko la namna bora ya kusimamia ubora wa bidhaa za nishati nchini pamoja na ukaguzi wake.



Meneja wa Mradi wa Utekelezaji wa Matumizi bora ya Nishati Tanzania, kutoka Shirika la Maendeleo( UNDP)Aaron Cunningham akizungumza na Wadau wakati Warsha ya Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Matumizi bora ya Nishati Tanzania inayofanyika tarehe 1hadi 3 Oktoba, Mkoani Morogoro.

"Azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kila mtanzania anapata nishati kwa uhakika, kwa gharama nafuu na uendelevu hivyo mafunzo kwa wadau mbalimbali ni muhimu ili kuchagiza utekelezaji wa haraka wa ajenda ya matumizi bora ya nishati." Amesisitiza Mha.Mruma

Kwa upande wake, Meneja wa Utekelezaji wa Matumizi Bora ya Nishati kutoka UNDP, Aaron Cunningham amesema uandaaji wa vigezo vya kitaalam na ujuzi katika kusimamia na kukagua matumizi ya nishati vinalenga kuandaa Wataalam ambao watasaidia nchi kufanya ukaguzi na usimamizi wa matumizi bora ya nishati.

"Warsha hizi ni endelevu na kwa kutumia warsha kama hii ya leo, tumeweza kupata miongozo mitatu kwa ajili ya kuandaa wataalamu hao. Miongozo hii itatumika nchi nzima na kutekelezwa na wadau mbalimbali wa nishati na elimu." Amesema Cunningham.

Ameongeza kuwa, UNDP kama mdau wa Maendeleo, itaendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania ili kuweka mazingira rafiki na rahisi katika masuala ya matumizi bora ya nishati pamoja na upatikanaji wake.



Mtaalamu wa Matumizi Bora ya Nishati, Sayuni Mbwilo kutoka Shirika la Maendeleo(UNDP) akizungumza na Wadau wakati wa Warsha ya Mpango wa Utekelezaji wa Matumizi bora ya Nishati, Tanzania kwa Wadau wa Nishati, inayofanyika tarehe 1hadi 3 Oktoba, Mkoani Morogoro.

# WASHIRIKI KONGAMANO LA JOTOARDHI AFRIKA WATEMBELEA VYANZO VYA JOTOARDHI

Picha mbalimbali zikionesha Washiriki wa Kongamano la Jotoardhi Afrika kutoka ndani na nje ya Tanzania wakiwa katika vyanzo vya Jotoardhi vya Ngozi, Kiejo-Mbaka na Songwe ikiwa ni sehemu ya programu za Kongamano la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) lililofanyika jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 21 hadi 27 Oktoba, 2024.














# PURA YATAKIWA KUJIPANGA TUKIO LA KUTANGAZA VITALU




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati (anayeshughulikia masuala ya mafuta na gesi), Dkt. James Mataragio akieleza jambo wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Pili wa Bazara la Pili la Wafanyakazi PURA uliofanyika Oktoba 21, 2024 Jijini Tanga

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati (anayeshughulikia masuala ya mafuta na gesi), Dkt. James Mataragio ametoa rai kwa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) kujipanga vyema kufanikisha tukio la kutangaza duru ya tano ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi nchini.

Dkt. Mataragio ametoa rai hiyo Oktoba 21, 2024 Jijini Tanga wakati wa ufunguzi wa Kikao cha Pili cha Mkutano wa Pili wa Baraza la Wafanyakazi PURA.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, Dkt. Mataragio ameiasa PURA kuhakikisha kuwa inajitoa kwa hali na mali kufanikisha tukio hilo muhimu kwa nchi ili kuweza kuvutia uwekezaji katika shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati (anayeshughulikia masuala ya mafuta na gesi) Dkt. James Mataragio (katikati - walioketi), Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi PURA Mha. Charles Sangweni (kulia kwa Mgeni Rasmi), Katibu wa Baraza Bw. Ebeneza Mollel (kushoto kwa Mgeni Rasmi), na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi PURA katika picha ya pamoja mara baada ya ufunguzi wa wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Pili wa Bazara la Pili la Wafanyakazi PURA uliofanyika Oktoba 21, 2024 Jijini Tanga.

"PURA mna kazi kubwa kama taasisi kuhakikisha kwamba hii licensing round inafanyika vizuri na tunapata matokeo mazuri" alisisitiza Mataragio.

Tukio la kutangaza duru ya tano ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini linatarajiwa kufanyika mwezi Machi, 2025 katika Kongamano na Maonesho ya Mafuta na Gesi Asilia kwa Afrika Mashariki litakalofanyika Jijini Dar es Salaam.

Kongamano hilo linaloandaliwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki linatarajiwa kuleta pamoja wadau zaidi ya 1000 kutoka ndani na nje ya Afrika Mashariki kwa lengo la kujadili uendelezaji endelevu wa rasilimali za mafuta na gesi asilia zilizopo katika nchi wanachama.

# UKARABATI KISIMA SONGO SONGO KUONGEZA UZALISHAJI GESI




Mkurugenzi Mkuu wa PURA Mha. Charles Sangweni akizungumza wakati wa ziara maalum katika Kitalu cha Songo Songo Mkoani Lindi ambako kazi ya ukarabati wa kisima cha uzalishaji wa gesi asilia unaendelea.

Ukarabati wa kisima cha gesi asilia unaoendelea katika Kitalu cha Songo Songo Mkoani Lindi unatarajiwa kuongeza uzalishaji wa gesi asilia kwa takribani futi za ujazo milioni 20 kwa siku.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Mhandisi Charles Sangweni wakati wa ziara ya kikazi aliyoifanya katika kitalu kicho Oktoba 27, 2024.

Mhandisi Sangweni alieleza kuwa kisima hicho kinachofanyiwa ukarabati kilipata changamoto ya kiufundi, hali iliyopelekea uzalishaji wa gesi asilia kutoka katika kisima hicho kisitishwa kwa muda.

Ukarabati huo utagharimu takribani Dola za Marekani Milioni 20 na unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwezi Novemba 2024.

"Ongezeko la futi za ujazo milioni 20 kwa siku unaotarajiwa mara baada ya kukamilika kwa ukarabati wa kisima hiki unaweza kuzalisha mpaka megawati 100 za umeme" aliongeza Sangweni.

Uzalishaji wa gesi asilia kutoka katika Kitalu cha Songo Songo ulianza mwaka 2004 kwa lengo kuu la kuzalisha umeme. Kitalu hicho kina jumla ya visima sita vya uzalishaji. Kwa robo ya kwanza ya mwaka 2024/24 uzalishaji wa gesi asilia kutoka katika Kitalu cha Songo Songo ulikuwa wa wastani wa futi za ujazo milioni 86 kwa siku.



Muonekano wa kisima namba 7 ambacho kinafanyiwa ukarabati katika Kitalu cha Songo Songo. Ukarabati huo utawezesha ongezeko la uzalishaji wa gesi asilia kwa takriban futi za ujazo milioni 20 kwa siku.



Muonekano wa kisima namba 7 ambacho kinafanyiwa ukarabati katika Kitalu cha Songo Songo. Ukarabati huo utawezesha ongezeko la uzalishaji wa gesi asilia kwa takriban futi za ujazo milioni 20 kwa siku.

# PURA YAFANYA ZIARA YA UFUATILIAJI EYASI-WEMBERE



Wataalamu wa PURA, TPDC na AGS katika picha ya pamoja mara baada ya ziara ya ufuatiliaji iliyofanywa na PURA katika Kitalu cha Eyasi-Wembere ambako kazi ya uchukuaji wa data za mitetemo za 2D za nyongeza (Infill and Additional 2D seismic data) inaendelea

Katika kutekeleza majukumu yake ya kisheria, Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) imefanya ziara ya ufuatiliaji katika Kitalu cha Eyasi Wembere ambako kazi ya uchukuaji wa data za mitetemo za 2D za nyongeza (Infill and Additional 2D seismic data) inaendelea

Awali, data za mitetemo za 2D katika Kitalu hicho zilichukuliwa mwaka 2023.Kazi ya uchukuaji wa data za nyongeza katika Kitalu cha Eyasi-Wembere ni mwendelezo wa programu ya utafutaji wa mafuta katika Kitalu hicho.

Uchukuaji wa data hizo utawezesha upatikanaji wa taarifa za kutosha kuhusu jiolojia ya Kitalu hicho. Taarifa hizo zitawezesha, pamoja na mambo mengine, uainishwaji wa maeneo ya kuchimba visima vya utafutaji wa mafuta.

Kazi ya uchukuaji wa data inatekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kupitia kampuni ya African Geophysical Services Limited (AGS). Hadi wakati wa ziara, utekelezaji wa kazi ulikuwa umefikia asilimia 20.

Kitalu cha Eyasi Wembere kinapatikana kaskazini mashariki mwa Tanzania katika Bonde la Ufa la Afrika Mashariki, tawi la Mashariki. Kitalu kina ukubwa wa kilomita za mraba 10,634.9. Eneo hilo limegusa mikoa ya Singida, Tabora, Shinyanga, Simiyu and Arusha.

# MAJIMBO KUMI (10) YA MKOA WA DODOMA KUSAMBAZIWA UMEME

- Uwekezaji huo utaigharimu Serikali shilingi bilioni 18 katika kipindi cha miaka miwili
- Kaya 4,950 zitanufaika na Mradi huo




Mkuu wa mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, (kulia) akimskiliza Msimamizi wa Miradi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Kanda ya Kati, Mhandisi Aneth Malingumu alipokuwa akimtambulisha mkandarasi, kampuni ya DETM Group (T) Ltd; iliyoshinda kandarasi ya Mradi wa Kusambaza Umeme kwenye vitongoji 150 vya majimbo kumi (10) ya mkoa wa Dodoma. Hafla ya kumtambulisha mkandarasi huyo ilifanyika Oktoba 18, 2024.

Mkuu wa mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, tarehe 18 Oktoba, 2024 amempokea rasmi, mkandarasi, kampuni ya DERM Group (T) Ltd; kampuni ya ndani, iliyoshinda kandarasi ya Mradi wa Kusambaza Umeme kwenye vitongoji 150 vya majimbo kumi (10) ya mkoa wa Dodoma; Mradi unaotarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka miwili, kuanzia sasa.

Katika hafla hiyo; Mhe. Rosemary Senyamule amemshukuru, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa shilingi bilioni 18.2 kwa ajili ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa Kusambaza Umeme kwenye Vitongoji (HAMLET PROJECT II) katika vitongoji 150 vya mkoa wa Dodoma ambapo Wateja wa awali wanaotajiwa kuunganishwa na huduma ya umeme, watakuwa 4,950.

"Mkoa wa Dodoma una jumla ya vijiji 580 ambapo kati ya hivyo vijiji 560 vimepata huduma ya umeme kupitia Miradi ya awali ikiwemo REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza, REA Awamu ya Pili na REA Awamu ya Kwanza. Aidha, kupitia Mradi wa REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili vijiji 20 viko katika hatua mbalimbali za kukamilishwa kwake (Vijiji 17 vya wilaya ya Mpwapwa na vijiji 3 vya wilaya ya Kondoa)". Amekaririwa Mhe. Senyamule.

Viongozi wa REA; wakiongozwa na Msimamizi wa Miradi Kanda ya Kati, Mhandisi, Aneth Malingumu amemwambia Mkuu wa mkoa wa Dodoma kuwa, vitongoji 1,631 kati ya vitongoji 2,892 sawa na asilimia 56 vimekwisha kupatiwa umeme kupitia Miradi mbalimbali ya Wakala (REA) na TANESCO. Sambamba na hivyo, vitongoji 150 vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa vitongoji vya majimbo kwenye mwaka huu wa fedha Fedha wa 2024/25. Aidha, vitongoji 1,111 vilivyosalia vitaendelea kupatiwa umeme kwa awamu nyingine na kulingana na upatikanaji wa fedha.

“Kwa sasa Wakala wa Nishati Vijijini unatekeleza jumla ya Miradi Mitatu (3) katika maeneo tofauti ya mkoa wa Dodoma yenye jumla ya shilingi bilioni 96.8. Gharama hii inajumuisha shilingi bilioni 18.22 za mkataba baina ya mkandarasi, kampuni ya DERM Group (T) Ltd uliosainiwa hivi karibuni, na mkandarasi wake tunamtambulisha leo kwako”.

“Mradi huu, unalenga kufikia vitongoji 150 vya mkoa wa Dodoma ambapo kila jimbo katika majimbo kumi (10) limepata jumla ya vitongoji 15. Kipaumbele cha mradi huu katika maeneo yatakayofikiwa ni huduma za kijamii yakiwemo mashule, hospitali, ofisi za serikali za mitaa pamoja na nyumba za ibada. Vilevile mradi huu utanufaisha kaya 4,950 na utatekelezwa kwa muda wa miezi 24.” Amesema, Mhandisi, Aneth Malingumu.

Majimbo hayo ni pamoja na Chamwino; Mvumi; Kongwa; Chemba; Kondoa Vijijini; Kondoa Mjini; Mpwapwa; Kibakwe; Bahi na Dodoma Mjini.

Naye, Mhandisi, Hadija Mukiza; Msimamizi wa Mradi huo kwa mkoa wa Dodoma amesema kampuni yao [DERM Group (T) Ltd] imejipanga ili kukamilisha Mradi wa kusambaza umeme kwenye vitongoji 150 vya mkoa wa Dodoma kwa haraka na wanataraji kumaliza kabla ya muda wa mkataba kuisha.

# BUKOMBE WAUNGA MKONO JITIHADA ZA RAIS SAMIA KUHUSU NISHATI SAFI YA KUPIKIA

- **ZAIDI YA MITUNGI 1,500 YATOLEWA KWA BEI YA RUZUKU**
- **DC BUKOMBE AMSHUKURU RAIS SAMIA NA AIPONGEZA REA**




Mkurugenzi wa Teknolojia za Nishati Jadidifu na Mbadala kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Advera Mwijage akitoa Semina maalum ya Nishati Safi ya Kupikia kwa wakazi wa Wilaya ya Bukombe Oktoba 10, 2024 ikiwa ni muendelezo wa kutoa elimu ya nishati safi kupikia.

Wananchi kote Nchini wametakiwa kuendelea kuunga mkono jitihada za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kutumia Nishati Safi ya Kupikia ili kuimarisha afya zao sambamba na kutunza mazingira.

Wito huo umetolewa Oktoba 10, 2024 Wilayani Bukombe na Mkurugenzi wa Teknolojia za Nishati Jadidifu na Mbadala kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Advera Mwijage wakati wa Semina maalum ya Nishati Safi ya Kupikia kwa wakazi wa Wilaya hiyo.

“Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kinara wa ajenda ya Nishati Safi ya kupikia na anafanya kila linalowezekana kuhakikisha kila mwananchi anapata bidhaa za Nishati Safi za kupikia kwa gharama nafuu”, alisema Mhandisi Mwijage.

Akizungumza wakati wa Semina hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, Mhe. Paskasi Muragili alimshukuru Rais Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa ruzuku kwenye bidhaa za nishati safi za kupikia suala ambalo alisema linakwenda kuimarisha afya za wananchi sanjari na kuhifadhi mazingira ambayo kwa kiasi kikubwa alisema yameathiriwa na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na

mkaa.

"Leo ni siku ya kihistoria kwa wakazi wa Bukombe, tunakwenda kupokea mitungi ya gesi kwa bei ya ruzuku na hizi ni jitihada za Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali anayoiongoza," alisema Mhe. Muragili.

Aliwasihi wananchi wote watakaojipatia mitungi hiyo kuhakikisha inapomalizika wanajaza ili kuendelea kutumia nishati safi ya kupikia na si kurejea katika matumizi ya kuni na mkaa.

Akizungumza wakati wa Semina hiyo, Mhandisi Mwijage alisema Wakala umepewa jukumu la kuhakikisha bidhaa za nishati safi za kupikia zinafika katika kila pembe ya nchi ili kumuwezesha kila mwananchi kuachana na matumizi ya nishati isiyo safi na salama.

"Serikali kupitia REA imeanza na itaendelea kutoa ruzuku kwa bidhaa za nishati safi za kupikia lengo ikiwa ni kuhakikisha hakuna mwananchi anaachwa nyuma," alisema.

Mhandisi Advera alisema kwa bidhaa za mitungi ya gesi (LPG) Serikali imeingia makubaliano na watoa huduma ya kusambaza mitungi na katika mikoa yoye nchini ambapo kwa awamu hii kiasi cha mitungi 452,445 itatolewa kwa bei ya ruzuku katika kila Mkoa

"Kwa hapa Bukombe, mtoa huduma atakayesambaza mitungi ni Kampuni ya Manjis ambapo mitungi hii ya kilo sita ikiwa kamili na kichomeo na figa itatolewa kwa shilingi 17,500 tu ambayo ni nusu bei, sawa na asilimia 50 tu ya gharama ili wananchi waweze kumudu gharama za nishati ya kupikia" Asilimia nyingine 50 inalipwa na serikali, alisema Mhandisi Mwijage.

Aliongeza kuwa upo mradi wa majiko banifu ambao wancho watachangia shingili elfu 5 hadi 15, na kwa sasa mradi huo upo katika hatua za uandaaji wa mikataba. Jumla ya majiko 200,000 yatasambazwa nchi nzima. Miradi mingine iliyotajwa ni pamoja na usambazaji wa gesi asilia,kuongeza uzalishaji wa mkaa Mbadala,kuwezesha taasisi zinazolisha watu zaidi ya watu 100 kutumia nishati safi pamoja na kutoa elimu kwa umma.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, Mhe Yusuph Yusuph alipongeza uwepo wa semina hiyo ambayo alisema itaongeza uelewa miongoni mwa wanamchi kuhusiana na suala zima la nishati safi za kupikia.

# REA INATEKELEZA MKAKATI WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA KWA VITENDO

- MITUNGI YA GESI (LPG) 452,445 KUSAMBAZWA KWA BEI YA RUZUKU
- KILA WILAYA KUPATA MITUNGI 3,255
- MAJIKO BANIFU 200,000 KUSAMBAZWA KWA RUZUKU YA HADI 75%



Meneja Usaidizi wa Kiufundi kwa Waendelezaji Miradi kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Emanuel Yesaya akimuelezea namna nishati za kupikia zinatumia umeme zinavyofanya kazi mmoja wa washiriki wa Kongamano la 10 la Jotoardhi (ARGeo-C10) lililofanyika Oktoba 22, 2024 Jijini Dar es Salaam.

Katika kuhakikisha asilimia 80 ya Wananchi wanatumia Nishati Safi za Kupikia ifikapo Mwaka 2034, Wakala wa Nishati Vijijini (REA) unaendelea na jitihada mbalimbali za uelimishaji, uhamasishaji na usambazaji wa bidhaa za Nishati Safi za Kupikia katika Mikoa yote Tanzania Bara.

Hayo yameelezwa Oktoba 22, 2024 Jijini Dar es Salaam katika Kongamano la 10 la Jotoardhi Afrika (ARGeo-C10) na Meneja Usaidizi wa Kiufundi kwa Waendelezaji Miradi REA, Mhandisi Emanuel Yesaya.

"Katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia, REA imeandaa program mbalimbali kuwezesha wananchi hasa wa maeneo ya vijijini kufikiwa na bidhaa mbalimbali za nishati safi za kupikia kwa gharama nafuu," amesema Mhandisi Yesaya.

Alisema program hiyo inahusisha usambazaji wa mitungi ya gesi ya kupikia (LPG) ya kilo 6 kwa bei ya ruzuku na kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025 kiasi cha mitungi 452,000 inasambazwa katika Wilaya zote Tanzania Bara kwa bei ya ruzuku ya asilimia 50.

Mhandisi Yesaya vilevile alibainisha kuwa kupitia program hiyo ya REA, jumla ya majiko banifu 200,000 yatauzwa kwa bei ya ruzuku ya hadi asilimia 75 chini ya ufadhili wa Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia.

"Tupo katika maandalizi ya kuanza kusambaza majiko banifu ambapo wananchi watachangia asilimia 25; kwa sasa mradi huu upo katika hatua za uandaaji wa mikataba na watoa huduma ambapo jumla ya majiko 200,000 yatasambazwa nchi nzima," alifafanua Mhandisi Yesaya.

Alisema Serikali inatambua umuhimu wa kulinda afya za wananchi wake sambamba na kuhifadhi mazingira ambayo kwa kiasi kikubwa yameathiriwa na matumizi ya Nishati chafu za kupikia zikiwemo kuni na mkaa na sasa mwelekeo ni kujikita katika matumizi ya Nishati Safi za Kupikia ambazo Serikali inafanya kila njia zifike kwa kila mwananchi

kwa gharama anayoweza kumudu.

"Hii ni fursa adhim ambayo imetolewa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye kinara wa Nishati Safi ya Kupikia kwa wananchi wake, tunatoa rai kwa Watanzania kuchangamkia fursa hii," alisema Mhandisi Yesaya.

Wakala wa Nishati Vijijini unashiriki Kongamano la 10 la Jotoardhi (ARGeo-C10) kwa kueleza mafanikio ya Serikali katika kusambaza umeme maeneo ya vijijini na sasa vitongojini, kuonyesha majiko ya kisasa yanayotumia nishati ya umeme sambamba na kutoa elimu kuhusiana na Nishati Safi za Kupikia kwa washiriki wa kongamano.

# REA YAANZA KUGAWA MAJIKO BANIFU KWA WANANCHI

- Yashiriki Samia Kilimo Biashara Expo 2024
- Kugawa majiko 790 Wilaya ya Gairo
- Yanatunza mazingira na rafiki kwa afya ya watumiaji



Mhandisi kutoka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Deusdedith Malulu akielezea namna ya kutumia majiko banifu kwa wananchi waliotembelea banda la REA wakati wa Maonesho ya Samia KILIMO Biashara Expo 2024 yaliyofanyika Wilaya ya Gairo, mkoani Morogoro Oktoba 6, 2024.

Imeelezwa kuwa, Majiko Banifu yanayotolewa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) katika Maonesho ya Samia KILIMO Biashara Expo 2024 yanapatikana kwa gharama nafuu, yanatunza mazingira, yanadumu na rafiki kwa afya ya watumiaji.

Hayo yamebainishwa leo tarehe 6 Oktoba, 2024 na Mkuu wa wilaya ya Gairo, Mhe Jabir Makame wakati akizungumza na wananchi alipotembelea banda la REA yanapofanyika maonesho hayo kwa msimu wa tatu mwaka huu kijiji cha Leshata wilaya ya Gairo mkoani Morogoro.

Mhe. Makame ameeleza kuwa, majiko banifu ni rafiki na salama kwa afya ya watumiaji nchini na kuwasisitiza wananchi wake wayatumie kwa kuwa yanauzwa na kupatikana kwa bei rafiki.

Makame amesema wananchi hao wanakwenda kushuhudia mageuzi makubwa ya utunzaji wa mazingira kupitia Mkakati wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ambao kinara wake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Amesema Gairo inatekeleza kampeni ya URITHI WA KIJANI yenye lengo la kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yana athari katika Sekta ya Kilimo na Mifugo.

Ametaja wadau wanaoshiriki kuwa ni pamoja na Mashirika ya Mazingira, Kampuni za Gesi, Kampuni zinazotengeneza mkaa mbadala ikiwemo STAMICO, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira pamoja na Wizara ya Nishati.

Naye, Mhandisi wa REA Deusdedith Malulu ameongeza kuwa, majiko hayo yanatunza mazingira kwa kutumia kiasi kidogo cha mkaa na ufanisi wake ni mkubwa.

"Majiko haya hayaruhusu hewa ya mkaa ambayo ni hatari kwa watumiaji kutoka nje kwa aina

ya muundo wake na hivyo kuwa rafiki kwa mazingira" amesema Mha. Maluku

Mha. Malulu amesema kupitia maonesho hayo wananchi wa wilaya hiyo wameanza kupatiwa majiko banifu na REA imeaza kutoa majiko 790 ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini.

# REA PAMOJA NA WADAU WAUNGA MKONO KAMPENI YA NISHATI SAFI

- Yashiriki Samia Kilimo Biashara Expo 2024
- Kugawa majiko 790 Wilaya ya Gairo
- Yanatunza mazingira na rafiki kwa afya ya watumiaji



Wananchi mbalimbali wakiwa wamejitokeza kununua mitungi ya gesi kwa bei ya ruzuku katika banda la Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wakati wa Maonesho ya Madini yaliyofanyika Mkoani Geita.

Wakala wa nishati Vijijini ( REA ) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Teknolojia za nishati safi wamuunga mkono Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha ifikapo mwaka 2034 asilimia 80 ya watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.

Ikumbukwe kwamba, hivi karibuni Mei 8 Mwaka huu 2024 katika ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa Julius Nyerere ( JNICC ) jijini Dar es salaam,Rais wa jamhuri ya Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua Mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia na kutoa maelekezo kwamba uundwe mkakati wa pamoja wa ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi katika utekelezaji wa mpango wa kuhamasisha upatikanaji na matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kufikia lengo hilo lililoanza mchakato wake tangu mwezi Novemba mwaka 2022.

Akizungumza na waandishi wa habari Kwa Niaba ya Mkurugenzi Mkuu Wa wakala wa Nishati Vijijini (REA) Kaimu Meneja wa usaidizi wa kiufundi kwa uendelezaji wa miradi, Mhandisi Emmanuel Yesaya amesema Wakala Umeitikia wito wa kauli mbiu ya maonesho isemayo "Matumizi ya Teknolojia sahihi na nishati safi katika Sekta ya Madini kwa maendeleo endelevu" na kukili kwamba kauli mbiu hiyo inaunga mkono dhima ya Rais wa Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhamasisha upatikanaji na matumizi ya nishati safi kwa maendeleo endelevu.

Mhandisi Yesaya amesema katika kuunga mkono jitahada za Mhe. Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhamasisha upatikanaji na matumizi ya nishati safi ya kupikia, Wakala umeleta majiko ya LPGs ambayo yanapatikana kwenye banda la REA kwa bei ya ruzuku ya shilingi 17,500 tu na mwanachi atatakiwa kuja na kitambulisho cha Taifa (NIDA).

Amesema serikali imeweka ruzuku hiyo ili kuwawezesha wananchi kuweza kumudu gharama ya ununuzi wa majiko hayo.

Mhandisi Yesaya ametoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Geita na mikoa jirani kujitokeza kwa wingi kushiriki kwenye maonesho na kuchangamkia fursa ya ununuzi wa majiko kwa bei ya ruzuku pamoja na kujifunza Teknolojia mbalimbali za nishati safi.

Kwa kufanya hivyo ni kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kampeni yake ya kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2034 asilimia 80 ya watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.



For more info
**www.nishati.go.tz**